Kuanzia Tarehe: May 1, 2007

Alifu Kuhusu Faragha ya Kawaida

Alifu hii huelezea jinsi habari kuhusu afya yako yaweza kutimiwa na kujulishwa wengine na jinsi waweza kupata habari hii.
Tafadhali soma kwa makini.

Kama una maswali kuhusu alifu hii, tafadhali wasiliana na *HowardCenter's Privacy Officer* katika 488-6900.

NANI ATAFUATILIA ALIFU HII

Alifu hii yaelezea mambo yetu ya kawaida na yale:

- Ya wenye kukupa majali welevu wenye ruhusa kuweka habari ya afya yako.
- Mahala yote ya huduma na vipindi vya HowardCenter.
- Wanaojitolea na tunawaoruhusu kukusaidia unapopokea huduma kutoka HowardCenter.
- Wafanyikazi wote, mmojawetu na wengine.
- Wote katika HowardCenter, makao, na vituo vyote hufuatilia maagizo ya alifu hii. Wote katika makao haya, vituo na mahala waweza kugawa habari ya afya katika wao wenyewe kwa kutibu, malipo au mambo ya uendeleaji kama invyoelezewa katika alifu hii.

AHADI YETU KUHUSU HABARI YA AFYA.

Tunaelewa ya kwamba habari ya afya yako na afya yako ni binafsi. Ni jukumu yetu kuweka habari ya afya yako iliwa binafsi. Sisi hutengeneza rekodi ya ujali na huduma unazopokea katika wakala. Twahitaji habari hii ili kukupea ujali mwema na kuambatana na mahitaji mengine ya kisheria. Alifu hii hutumika katika rekodi zote za majaliwa inayotolewa na wakala, iwe imetengenezwa na wenye wakala au dakitari wako. Dakitari wako wa kibinafsi aweza kuwa na sera tofauti au alifu kuhusu matumizi ya dakitari na ujulishaji wa habari ya afya yako iliyotengenewa katika afisi ya dakitari au zahanati.

Alifu hii itakuelezea njia ambazo tunaweza kutumia na kujulisha habari ya afya yako. Pia tunaelezea haki zako na jukumu zetu kuhusu utumiaji na ujulishaji wa habari ya afya.

Tunatakikana katika sheria ku:

- Hakikisha habari ya afya yako imewekwa binafsi.
- Kukupa alifu hii ya jukumu zetu katika sheria na ubinafsi kususu afya yako; na
- Kufuata maagizo ya alifu ambayo imo kwa wakati huu.
- Kufuata sheria za jimbo ambazo ni kali au kukupatia haki zaidi ya alifu hii.

JINSI TWAWEZA KUTUMIA NA KUJULISHA HABARI YA AFYA YAKO.

Zifuatazo ni njia tofauti kuelezea jinsi tunavyotumia na kujulisha habari ya afya. Katika kila njia ya matumizi au ujulishaji tutaelezea maana na kupatia mifano. Sio kila matumizi au ujulisho zitaelezewa.

- **Kwa Kutibu.** Twaweza kutumia habari ya afya yako kukutibu au katika huduma. Twaweza kujulisha hali yako kwa madakitari, wauguzi, wenye zahanati, meneja wa kesi, wasaidizi au watu wengine katika wakala wanaohusika kukuhudumia. Kwa mfano wenye zahanati waweza kuwa wanakutibu katika kasoro za akili na wangetaka kuwasiliana na madakitali wetu wa kichwa au wanazahanati wengine wenye elimu zaidi katika mambo fulani ya ujali. Pia twaweza kujulisha habari yako kwa watu nje ya wakala wanaohusika katika ujali wa afya yako.

- **Kwa Malipo.** Twaweza kutumia na kujulisha habari ya afya yako ndio matibabu na huduma unazopokea katika wakala idhiniwe na, ihundiwe kwa, na malipo kuchukuliwa kutoka kwa wengine kama kampuni ya bima au kamati ya usaidizi wa huduma za uendeleaji. Kwa mfano, tungetaka kupatia mpangilio wa habari kuhusu mashauri uliyopata katika wakala ndio mpangilio wa afya yako uweze kulipa sisi au urudishiwe malipo ya kipindi cha mashauri uliopokea. Twaweza kujulisha mpangilo wa afya yako kuhusi matibabu utakayopokea kabla kuridhiwa au kuhakiki kama mpangilio wako utasimamia huduma/matibabu.

- **Kwa Mambo ya Ujali wa Afya.** Twaweza kutumia au kujulisha habari ya afya yako kwa uendeshaji wa wakala. Matumizi haya na majulisho ni muhimu kwa kwa kuendelesha wakala na kuhakikisha wanakopata huduma kutoka kwetu wanapata ujaliwa bora. Kwa mfano, twaweza kutumia habari ya afya kuangalia matibabu yetu na huduma na kuhakiki utendaji wetu katika kukuhudumia. Tunaweza pia kukusanya habari ya afya kuhusu watenha lujadiliana na huduma za nyongeza tunazopeana, huduma gani zinahitajika, na kama matibabu fulani mapya ni thabiti. Tunaweza kujulisha habari kwa madaktari, wauguzi, wanacliniki meneja wa kesi, waliojitolea na wengine katika wakala ili kuangalia tena na kusoma.

  Twaweza pia kukusanya habari ya afya tuliyo nayo na habari ingine ya afya kutoka kwa wakala zingine za afya ya akili ili kulinganisha vyenye tunafanya na kuangalia mahala ambapo tunaweza kuboresha katika huduma tunazopeana. Tutatoa habari ambayo inayo onyesha wewe katika haya makundi ya habari ya afya ili wengine waweze kuitumia kusoma ujali wa afya na upatikanaji wa ujali wa afya bila kujua washitiri hawa ni kina nani.

- **Wakala ya Huduma za Binadamu.** Wakala hii imetengenezewa *Community Mental Health Agency* na Vermont na ina jukumu katika kandarasi yake pamoja na *Vermont Agency of Human Services* kwa kupatia huduma kadha wa kadha. Kwa matokeo, *Agency Human Services* yaweza kupata nafasi ya kuona habari ya afya iliyohusiana na huduma zilizo katika kandarasi kwa niaba ya kupata matibabu kwa wateja, malipo au kwa anjiri ya uendelezaji wa ujali wa afya.

- **Ukumbusho wa Madaraka.** Twaweza kutumia na kujulisha habari ili kukufikia na kukumbusha kwamba una madaraka au appointment.

- **Matibabu Mengine na Faida na Huduma.** Tunaweza kutumia na kujulisha habari kuhusu wewe ndio tupate na kukupendekeza matibabu mengine ya hiari na huduma zilioko pamoja na manufaa mengine yanayohusu afya.

- **Utenzi wa Michango.** Kama haja ikipatikana ya habari yako au usaidizi wako unatakikana kwa anjiri ya utenzi wa michango, wakala itakuomba ruhusa**.**

  Hakuna habari itatolewa kwa sababu hii bila ruhusa kutoka kwako. Kwa mfano, kama wakala ingetaka kutengeneza picha na makaratasi au maoni kutoka kwa mtu ambaye amehudumiwa ili kufanya michango, wakala itauliza kama utajitolea kushirikiana. Kushirikiana huwa ni kujitolea, na kama umekubali, utaulizwa kutuandikia barua ya kukubari kawa maana haya maalum.

- **Utafiti.** Wakati mwingine, twaweza kutumia na kujulisha habari ya afya yako kwa niaba ya utafiti. Kwa mfano, mpango wa utafiti waweza kuhusu kulinganisha afya na uwezo wa kupona ya washitiri wote waliopata dawa fulani baina ya wengine waliopata dawa ingine kwa anjiri ya ugonjwa mmoja. Mipango yote ya utafiti, lakini, lazima ipate idhini maalum. Mipango hii hupima pendekezo za mipango ya utafiti na matunizi yake katika habari ya afya, na kujaribu kutoshanisha mahitaji ya utafiti na ya washitiri kwa anjiri ya ubinafsi wa habari ya afya yao. Kabla tuitumie au tujulishe habari ya afya kwa utafiti, mpango lazima uthibitishwe kupitia kwa mpango wa idhini wa utafiti lakini, tunaweza kujulisha habari ya afya yako kwa watu wanaojitayarisha kufanya mpango wa utafiti, kwa mfano kuwasaidia kutafuta washitiri ambao wana mahitaji ya kiafya maalum, ikiwa habari ya afya wanayopitia haitoki wakala. Tutakuwa tukikuomba ruhusa maalum kila mara kama wenye kufanya utafiti watapata nafasi ya kuona jina lako, anwani au habari nyingine inayoonyesha wewe ni nani, au itahusiana na ujali kwako katika wakala.

- **Kama Itakikanavyo Katika Shelia.** Tutajulisha habari ya kiafya yako kama inatakikana katika sheria za nchi, jimbo, na mkoa. Katika jimbo la Vermont, itakuwa pamoja na; watoto walioathiliwa na kudhulumiwa, safihi, kuzembea au dhuruma kwa watu wazima wasio na nguvi, au kwa mtoto asiyezidi miaka mikumi na sita aliyefanyiwa ujinai; na majeraha iliyosababishwa na bunduki. Wakati mwingine, wakala ya *Human Services* imepewa jukumu ya kuangalia habari ya afya ili kuendeleza jukumu na biashara zake.

- **Kuzuia Vitisho Vikali Kwa Afya au Usalama.** Tunaweza kutumia na kujulisha habari za afya yako kama itakikanavyo kuzuia vitisho vikali kwa afya yako na usalama au afya na usalama kwa umma au mtu mwingine. Julisho lolote, lakini, itakuwa kwa mtu mwenye kuzuia hivyo vitisho.

HALI MAALUM

- **Wanajeshi na Waliokuwa Majeshi Katika Vita.** Kama wewe in mmoja wa waliokuwa katika jeshi, tunaweza kuonyesha habari ya afya yako kama itakikanavyo na wanajeshi wenye mamlaka katika amri.

- **Malipo kwa wafanyikazi walioadhilika.** Tunaweza kupatiana habari ya afya yako kama ilioruhusiwa kwa malipo kwa wafanyikazi waliopata majeraha kazini au mipangilio mingine kama hivyo kama ilivyokubaliwa na sheria za jimbo la Vermont. Mipango hii hupatia manufaa kwa majeraha iliyofanyika kazini au magonjwa.

- **Hatari Kwa Afya ya Uma.** Tunaweza kujulisha habari ya afya yako juu ya utenzi wa afya ya uma. Utenzi huu sana sana huwa unahusika na haya:

  - Kuzuia au kupunguza maradhi, ajali au kutojiweza;
  - Kutangaza kufo;
  - Kushtaki kuzembea kwa watoto au usafihi.
  - Kushtaki kuzembea, usafihi, kunyanyaswa kwa watu wazima wasio na uwezo; kushukiwa kwa usafihi wa aina yoyote, kuzembea, au kunyanyaswa kwa watu wakongwe (miaka 60 au zaidi), au watu wazima wasiojiweza ambao wamepatikana na shida za kimwili au akili, lazima yashtakiwe.
  - Kushtaki shida kutikana na madawa au kasoro kwa bidhaa;
  - Kujulisha watu bidhaa mbaya zirudishwe ambazo wangetumia;
  - Kujulisha mtu ambaye awezakuwa amekumbwa na ugonjwa au angekuwa hatarini kwa kuambukizwa au kueneza ugonjwa au shida.

- **Mambo ya Kuangalilia Afya.** Tunaweza kujulisha habari ya afya kwa wenye kuangalilia mambo ya afya kama vile *Agency of Human Services*, kwa mambo yaliyoruhusiwa na sheria. Haya mambo ya kuangalilia ni pamoja na, lakini siyo hayo tu, kuangalia hesabu, uchunguzi, ukagazi na uruhusiwa. Mambo haya hutakikana kwa serikali kuangalia mfumo wa ujali wa afya, miradi ya serikali, na ushilikiano wa haki za binadamu katika sheria.

- **Mashtaka ya Kisheria na Mizozo.** Kama umehusika katika mashtaka au mizozo, tunaweza kujulisha habari ya afya yako kutokana na amri ya koti au amri ya utawala.

- **Afisa wa Afya ya Uma na Wakurugenzi wa Vyumba Vya Mazishi.** Twaweza kuwapatia habari wachunguzi wa maafa au madaktari wachunguzi. Hii huhitajika, kwa mfano, kutambua maiti, au kuhakiki kilichosababisha kifo. Tunaweza kujulisha habari ya afya kwa wakurugenzi wa vyumba vya mazishi ili kuwawezesha kuendeleza kazi yao.

- **Walioko katika jela.** Kama wewe ni mmahabusu wa jela au kulingana na ufungwa wa polisi, tunaweza kupatiana habari ya afya yako katika jela au kwa afisa wa polisi. Kupatiana huku kutasaidia (1) upate matibabu kutoka kwa jela; (2) kubinafsisha afya yako na usalama au afya na usalama kwa wengine; au (3) kwa usalama na ulinzi wa jela au gereza.

MATUMIZI MENGINE YA HABARI YA AFYA

Matumizi mengine au kuachilia habari ya afya iliyo patikana katika ilani hii au sheria zilizomo kwetu zitafanyika tu kwa ruhusa yako kwa maandishi. Ukitupatia ruhusa kupitia maandishi

kutumia au kujulisha habari ya afya yako, unaweza kufuta ruhusa hiyo, kwa maandishi, wakati wote. Ukifuta ruhusa, hatutaweza kutumia au kupatiana habari ya afya yako kwa sababu utakazoelezea katika maandishi ya ruhusa. Unaelewa ya kwamba hatuwezi kurekebisha yale tuliyopatiana hapo awali kwa ruhusa kutoka kwako, na kwamba tunatakiwa kuweka habari ya huduma tuliokupa.

HAKI ZAKO KUHUSU HABARI YAKO

Msaada wowote (hali, uwasiliano, na kadhalika) ungetaka ili upate haki zako, utapata kutoka kwa HowardCenter.

Una haki zifuatazo kuhusiana na habari ambayo tumeweka kuhusu wewe:

- **Haki ya kusoma na Kuandika Mahali Pengine.** Una haki ya kusoma na kuandika habari ya afya yako mahari pengine ambayo yaweza kutumiwa kukata shauri kuhusu ujali wako. Hii inaweza kuwa afya na uhundi.

  Kusoma na kuandika habari kuhusu afya ambayo yaweza kutumiwa kukata shauri kuhusu wewe, ni lazima uulize kwa njia ya barua kwa wanazahanati au *Health Information Department* (HowardCenter, 300 Flynn Ave Burlington, VT 05401) Kama ungetaka habari hiyo kwa karatasi yako binafsi, tunaweza kukutosha pesa ya kutoa, kutuma au matumizi mengine inayohusiana na mahitaji yako.

  Tunaweza kukunyima au kukuwekea vikwazo jinsi kupata habari hiyo, kusoma na kuandika mahali pengine kwa sababu zingine chache sana. Kama ukunyimwa au kuwekewa vikwazo kuona habari ya afya yako, unaweza kuomba kauli hiyo iangaliwe tena. Mfanyi kazi wa ujali wa afya mwingine mwelevu aliyechaguliwa na wakala ataangalia maombi yako na hali ya kunyimwa. Mwenye kuangalia hawezi kuwa ndiye mwenye kukunyima. Tuafuata matokeo ya uangalifu.

- **Haki ya Kubadilisha.** Ukifikiria kwamba habari ya afya tuliyo nayo kuhusu wewe si ya kweli au sio kamilifu, unaweza kutuabia tubadilishe habari hiyo. Una haki ya kuomba kubadilishwa ikiwa habari hiyo imewekwa na, au kwa anjiri ya wakala.
  Ndio uombe kubadilishwa, ombi lako lazima iwekwe kwa maandishi na kupatiwa mwandishi wa sehemu ungetaka ibadilishwe au kwa *Health Information Department* (HowardCenter, 300 Flynn Ave Burlington, VT 05401).Tena, ni lazima uonyeshe sababu ya kusaidia ombi lako.

  Tunaweza kukataa ombi lako la kubadilisha kama haiko kwa maandishi au haina sababu ya kusaidia ombi lako. Tena, tunaweza kukataa ombi lako kama ukituuliza tubadilishe habari ambayo:

  - Haikutengenezwa na sisi, isipokuwa mwenye kutayarisha habari hiyo hawezi kupatikana kufanya marekebisho.
  - Siyo sehemu ya habari sio sanifu ambayo imewekwa na wakala
  - Sio sehemu ya habari ambayo ungeruhusiwa kuona au kuandika; au,
  - Ilipatikana kuwa sanifu au kamili na wakala.

- **Haki Ya Hesabu ya Kujulisha.** Una haki ya kuomba "hesabu ya kujulisha." Hii ni orodha ya ujulisho tuliofanya ya habari ya afya yako ambayo inahitajika katika sheria na/au haikuruhusiwa na wewe.

  Ndio uombe orodha hii au hesabu ya ujulisho, lazima uulize kwa maandishi kwa *Health Information Department* (HowardCenter, 300 Flynn Ave Burlington, VT 05401). Ombi lako lazima ionyeshe wakati, ambayo haiwezi kuzidi mda wa miaka sita na haiwezi kuwa na tarehe kabla Aprili 14, 2003. Ombi lako lazima ionyeshe mfano ya orodha unayotaka.(kwa mfano, katika karatasi, kwa njia ya kutimia sitima) Ordha ya kwanza utakayo omba katika mda wa miezi 12 ni bure. Kwa orodha nyingine nyongeza, tunaweza kukutosha kwa gharama ya kutoa orodha. Tutakujulisha kuhusu malipo na unaweza kuamua kutangua au kugeuza ombi lako wakati huo kabla gharama ipatikane.

- **Haki Ya Kumomba Vikwazo.** Una haki ya kuomba kuwekewa vikwazo katika habari ya afya ambayo tumatumia au tunayojulisha wengine kuhusu wewe kwa anjiri ya matibabu,malipo au mambo ya ujali wa afya. Sio lazima tukubali ombi lako. Kama tukikumbali, tutafuata ombi lako isipokuwa habari hiyo inatakikana ili kukupea matibabu ya dhalula. Pia una haki ya kuuliza kuwekwa mwisho katika habari ya afya ambayo tunapeana kuhusu wewe kwa mtu ambaye anashughulika na ujali wako au malipo ya ujali wako, kama mtu kutoka jamii. Kwa mfano, unaweza kutuuliza kuacha kutumia au kupatiana habari kuhusu kipindi cha ushauri uliopata

  Ili kuomba kuwekwa mwisho, ni lazima uweke ombi lako katika maandishi kwa mfanyikazi wa kukukaribisha au mwanazahanati. Katiaka ombi lako, ni lazima utueleze ya kwamba (1) ni habari gani ungetaka iwekwe mwisho; (2) kama ungetaka kuweka mwisho utumiaji wetu, ujulishaji au zote mbili; na (3) Ni kwa nani ungetaka iwekwe mwisho, kwa mfano, kujulisha bwana au bibi yako.

- **Haki ya Kuomba Mawasiliano ya Siri.** Una haki ya kuomba kwamba tuwasiliane nawe kuhusu mambo ya afya kwa njia fulani au katika mahali fulani. Kwa mfano, unaweza kutuuliza tukuongeleshe kazini au kwa barua pepezi.

  Katika kuomba mawasiliano ya siri, ni lazima uweke ombi lako katika maandishi kwa mfanyikazi wa kukaribisha au mwanazahanati. Hatutakuuliza sababu ya ombi lako. Tutafadhili maombi yako yote ya uwiano. Ombi lako ni lazima ionyeshe jinsi ya kukupata au wapi.

- **Haki ya Kupata Karatasi ya Nakala ya Alifu Hii.** Una haki ya kupata karatasi ya nakala ya alifu hii. Unaweza kutuuliza kukupatia nakala ya alifu iliomo wakati wowote.

  Ukitaka karatasi ya nakala ya alifu hii, wasiliana na *HowardCenter Privacy Officer* katika 488-6900

USALAMA WA HABARI YA AFYA.

Kwa sababu ya tabia ya mambo ya huduma za kibinadamu, wasimamizi wa wakala waweza kuwa na habari inaonekana binafsi zaidi ya usalama wa wakala. Katika kesi kama hizi,

wasimamizi wa wakala watahakikisha kwamba usalama na hali ya siri ya habari iko kwa njia ambayo ni ya kiwango cha sera ya wakala, jimbo na nchi.

SERA YA UBINAFSI WA MDAHALISHI KATIKA HowardCenter.

Ubinafsi wa wateja ni muhimu kwa HowardCenter. Tunaelewa ya kawamba wageni wa HowardCenter.org wanafaa kuwa na ubinafsi wa habari yao ya kibinafsi. Kwa hivyo, hii ndio sera ya ubinafsi wa mdahalishi katika HowardCenter:

- Sio lazima uweke habari ya ubinafsi wakao katika mtandao wao wa internet. Ukiamua kutoweka habari ya ubinafsi, bado utaweza kuingia katika kurasa zote za HowardCenter.

Cookies

Cookie ni nini?
Hii ni sehemu kidogo ya habari ambayo inatumwa katika compyuta yako — pamoja na kurasa -- katika mtandao wa internet. Kuna aina mbili za cookies. Kipindi kimoja cha cookies ni mstari wa maandishi ambayo imewekwa kwa mda katika compyuta. Kwasababu kipindi cha cookie haitawekwa katika chombo cha compyuta kilicho ndani, kinaharibiwa wakati unatoka kwa mtandao. Cookie ya kudumu ni mstari mgumu kidogo wa maandishi ambayo inanusuru ndani ya mtandao katika faili ndani ya hard drive.

HowardCenter haitumii hizo cookies.

Kuchanga data au habari

- Tunaweza kuchukua habari inayojulikana (jina, barua pepesi, anwani, na mambo mengine ya kukutambua) ila tu iwe maalum na umepeana kama ukujua.
- Habari iliyochukuliwa ni ya statistics nambari tu.HowardCenter huangalia mambo ya tabia ya mtumiaji ili kupima maslahi katika mahali mbali mbali vituo vyetu. HowardCenter pia hutumia listservs kutuma habari na kubadilisha alifu kwa waliojiandikisha na wanatumia mitandao yetu.
- HowardCenter italinda habari ya kibinafsi ambayo unagawa kwetu. HowardCenter haijulishi, kupatia, kuuza, au kuhamisha habari yoyote binafsi kwa watu wengine. Ikiwa tunagawa habari na watu wengine, tutawapatia habari kwa jumla tu.

Baura-Pepesi au E-Mail

Wakati HowardCenter itajaribu iwezekanavyo kulinda habari ya ubinafsi unayotupatia, baura pepesi sio salama dhidi ya kupatikana na wengine. Kama uwasiliano wako ni siri, ungetaka kutumia kwa barua ya posta.

Tungetaka uelewe: Hatuachukua habari binafsi ambayo inakutambulisha wakati utakapotutembelea katika mtandao wa internet, isipokuwa umechagua kutupatia habari kama hiyo.

KUBADILISHA ALIFU HII

Tuna haki ya kubadilisha alifu hii. Tuna haki ya kutengeneza alifu iliyorekebishwa au kubadilisha mwanzo wa alifu kwa habari ya afya tuliyo nayo kuhusu wewe pamoja na habari yoyote tutapata nyumaye. Tutatuma kwa njia ya posta nakala iliyomo katika mahali pote pa wakala. Alifu itakuwa na tarehe ya kuanzia katika kila kurasa, juu katika mkono wa kulia wa kurasa. Pia, tukubadilisha jambo kwa alifu hii, kabla ya tarehe ya kuanzia, tutachapa tangazo ya ubadilisho katika mahali pote pa wakala, katika mtandao wetu wa internet na katika gazeti ya mji.

MALALAMIKO

Kama ukifikiria haki zako za ubinafsi zimehalifiwa, unaweza kupeleka malalamiko kwa wakala au kwa Katibu au *Secretary of the United States Department of Health and Human Services*. Ndio uweze kupeleka malalamiko kwa wakala, wasiliana na:

Simu ya malalamiko au Complant Hot-line by phone at (802)-488-7195 au barua pepesi kwa compliancecomplaint@howardcenter.org

Katibu wa HHS anaweza kufikiwa kupitia ofisi zao za mji wa karibu katika Office of Civil Rights, *U.S. Department of Health and Human Services, Government Center,* J.F Kennedy Federal Building- Room 1875, Boston, Massachusetts 02203, simu ya sauti (617) 565-1340, fax (617) 565- 3809, TDD (617) 565- 1343.